**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

**Simu Na:** +27 2643068
+27 2644530/3
**Nukushi:** +255 27 2644141/27
2647905
**Barua Pepe**: info@tangacc.go.tz
**Tovuti:** www.tangacc.go.tz
**Unapojibu tafadhali taja:**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la
Tanga,
Barabara ya Hassani
Ngwilizi,
S. L. P. 178,
**TANGA.**

**Kumb.Na. TCC/S.20/12/C/35** **25/10/2021**

# TANGAZO LA KAZI

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA ANAPENDA KUTANGAZA NAFASI ZA KAZI KWA WATANZANIA WOTE WENYE SIFA KAMA IFUATAVYO:-**

1. **DEREVA II - MSHAHARA TGSB : Nafasi 2**

**Sifa za kuajiriwa**:
Waombaji wawe na cheti cha mtihani wa kidato cha IV wenye Leseni ya Daraja E au 'C1 ya uendeshaji magari pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali. Wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja II kutoka Vyuo vya udereva vinavyotambuliwa na Serikali.

**Kazi na majukumu:**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
vi. Kufanya usafi wa gari na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na Msimamizi wako.

iv. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu,
v. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk.) katika mafaili
vi. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali
vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI WOTE:**

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45
2. Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya paspoti saizi iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya muombaji na namba ya simu.
3. Watumishi waliowahi kuajiriwa Serikalini na kupata Cheki Namba hawataajiriwa tena bali wataajirwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
4. Juu ya bahasha aandike kazi aliyoomba,
5. Transcript na provision result havipokelewi
6. Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 178,
**TANGA.**

7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 08/11/2021 saa 9.30 mchana.

Sipora J. Liana
**MKURUGENZI WA JIJI**

MKURUGENZI WA JIJI
TANGA